

DAISY CENTRE AND SCHOOL

P.O BOX 1485-50100,

KAKAMEGA-KE

KAZI YA LIKIZO DARASA LA SITA 2020

KISWAHILI

SARUFI

Vitenzi katika kauli ya kutendewa

-Vitenzi ni maneno yanayoeieza kitendo kilichofanyika kwa mfano lima, cheza, pika, enda , cheka, keti n.k

Kutendewa ni mnyambuliko wa kitenzi tenda ambao una maana kwamba kitendo kimetendwa kwa niaba au kwa ajili ya mtu mwengine kwa mfano;

Mkulima alilimiwa shamba kubwa-kumaanisha mkulima alitendewa kitendo cha kulimiwa shamba.

Mifano Zaidi

Mvulana alinunuliwa saa mpya

Mimea ilimwagiwa maji mengi

Msichana alitafutiwa mchumba na wazazi wake

-Pia tunaweza kubadili mpangilio wa maneno katika sentensi ili kuweka kitenzi katika kauli ya kutendewa bila kubadili maana yake.

Mifano

Mzazi wangu alinifufulia nguo- Nilifuliwa nguo na mzazi wangu.

Rafiki yangu alinibeeba mkoba- Nilibebewa mkoba na rafiki yangu.

Baba alimshangilia mwanawe- Mwana alishangiliwa na babaye.

Amenipigia simu- Nimepigiwa simu naye.

Choma taka zote hapa- Taka zote zichomewe hapa.

Zoezi la kwanza

Kiswahili mufti darasa la sita kitabu cha mwanafunzi uk 70 na 72

Badili vitenzi vifuatavyo uvitie katika hali ya kutendewa

1. Furahi-
2. Tembea-
3. Lia-
4. Pika-

5. Ona-

Zoezi la pili

Andika kauli hizi katika hali ya kutendewa

Mfano

Amenipigia simu-Nimepigiwa simu naye.

- 1) Musa amemsaidia Juma.
- 2) Nimemkatia ngómbé nyasi.
- 3) Walimu wanamhitaji mtukutu.
- 4) Tutazifua nguo kesho.
- 5) Umeniondolea shida zangu.
- 6) Mama alimshangilia mwanawe.
- 7) Wanafunzi wanakifurahia kitabu.
- 8) Ukimwi unatutisha.
- 9) Wasimpigie mgonjwa kelele.
- 10) Choma taka zote hapa.

***** STAY SAFE*****

